

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BUNGE LA TANZANIA**

*Simu:* +255 026 23222761-5  
*Fax No.* +255 026 2322624  
**E-mail:** [cna@bunge.go.tz](mailto:cna@bunge.go.tz)



Ofisi ya Bunge,  
S.L.P. 941,  
**DODOMA.**

**TAARIFA KWA UMMA**

Kamati za Kudumu za Bunge zitaanza kukutana Jumatatu tarehe 16 hadi 29 Januari, 2023 Jijini Dodoma. Kamati hizo zinakutana kabla ya Mkutano wa Kumi wa Bunge uliopangwa kuanza tarehe 31 Januari, 2023.

Aidha, Kamati Mbili (2) zitaanza vikao tarehe 9 Januari, 2023. Kamati hizo ni Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI.

Shughuli zilizopangwa kufanywa na Kamati katika vikao hivyo ni kama ifuatavyo:-

- (a) Kupokea na Kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa za Mwaka za Shughuli za Kamati zilizowasilishwa Bungeni Mwezi Februari, 2022.
- (b) Kupokea na Kujadili Taarifa mbalimbali kuhusu Shughuli za Umma nchini ili kufuatilia utekelezaji wa sera na mipango ya sekta zinazohusika.
- (c) Kuchambua Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Kaguzi Maalumu na Kaguzi za Ufanisi. Shughuli hii imepangwa na Kamati mbili za Kudumu za Bunge za kusimamia matumizi ya fedha za umma.
- (d) Kupokea na kuchambua Taarifa za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ili kubaini iwapo uwekezaji huo una ufanisi na kuwa umezingatia taratibu, sheria na miongozo mujarabu ya biashara.
- (e) Kupokea na Kujadili Taarifa kutoka kwenye Wizara na Taasisi mbalimbali kuhusu Ukusanyaji wa Mapato, Usimamizi wa Vyanzo vya Mapato na Utekelezaji wa Bajeti.

- (f) Kamati ya Sheria Ndogo itachambua Sheria Ndogo zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa Tisa wa Bunge. Vilevile Kamati hiyo itapokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Tano, Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba wa Bunge.

Ratiba za Shughuli za Kamati zote inapatikana katika Tovuti ya Bunge ambayo ni [www.bunge.go.tz](http://www.bunge.go.tz).

**Imetolewa na:-** Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa,  
Ofisi ya Bunge,  
S.L.P 941,  
**DODOMA.**

5 Januari, 2023.